**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA PILI

**28 JANUARI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA PILI – TAREHE 28 JANUARI, 2015

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI MKUU:

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

Toleo Namba 45 – 49 ya Mwaka 2014, na Toleo Namba 1 la Mwaka 2015.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:

Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa kipindi cha Januari, 2014 hadi Januari, 2015.

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**15. MHESHIMIWA MCH. PETER SIMON MSIGWA (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kwa Mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji zinapaswa kutoa asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya Vijana na Wanawake:-

Je, agizo hilo la Kisheria limetimizwa kwa kiwango gani katika Halmashauri hizo.

**16. MHESHIMIWA DKT. GOODLUCK JOSEPH OLE – MEDEYE (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mwaka 2012 Serikali ilipandisha hadhi kilichokuwa Kituo cha Afya cha Olturumet kilichoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuwa Hospitali ya Wilaya na kuzinduliwa na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 1/11/2012 lakini hospitali hiyo haina jengo kubwa la maabara, nyumba za watumishi, lakini pia haina huduma ya x-ray hivyo wagonjwa hulazimika kufuata huduma hiyo Arusha Mjini:-

(a) Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kuanzisha huduma ya x-ray kwenye hospitali hiyo na kuondoa adha inayowapata wagonjwa kufuata huduma hiyo mjini;

(b) Je, ni lini Serikali itayashughulikia masuala ya maabara na nyumba za watumishi katika hospitali hiyo.

**17. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-
Wakulima wa Tumbaku wamekuwa wakitozwa ushuru wa asilimia tano (5%) ambayo hupewa Halmashauri husika; watu wengi wamependekeza ushuru huo kupunguzwa hadi asilimia mbili (2%) na ile asilimia tatu (3%) imrudie mkulima mwenyewe:-

Je, Serikali iko tayari kutekeleza pendekezo hilo.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**18. MHESHIMIWA VICENT JOSEPHAT NYERERE (MUSOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-
Uwanja wa Ndege wa Musoma ni mmoja kati ya viwanja kumi vilivyotakiwa kukarabatiwa na kuwekewa lami:-

Je, kazi hiyo itaanza lini.

## WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

**19. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH BUKWIMBA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme kwenye Taasisi za Umma zilizoko katika Jimbo la Busanda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

**20. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali ina Mamlaka ya kutwaa ardhi na kubadilisha matumizi ikiwa ni pamoja na kusimamia na kuhakikisha kuwa Wananchi wanaopisha matumizi mapya ya ardhi wanalipwa fidia na kupewa maeneo mbadala:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeruhusu shughuli za uchimbaji wa Madini katika eneo la Nyabigena zinazofanywa na Kampuni ya BARRICK bila kujali afya za Wananchi kwa kuwapa maeneo mbadala ikiwemo na shule

ya msingi Nyabigena ambao wanapata madhara makubwa;

(b) Je, Serikali inawaambia nini wakazi wa maeneo ya Nyamichele, Murambwe ambao licha ya kufanyiwa tathmini tangu mwaka 2012/2013 bado Mwekezaji hajawalipa fidia husika kama Sheria inavyoelekeza;

(c) Je, Serikali imeshindwa kusimamia zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi wanaozunguka Mgodi wa North Mara ambao wanapewa fidia ndogo kuliko uhalisia wake.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 21. MHESHIMIWA DKT. AUGUSTINO LYATONGA MREMA (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-Ukanda wa nusu maili kuzunguka Mlima Kilimanjaro ulitolewa kwa Wananchi kwa ajili ya kukata majani na kuokota kuni:-

Je, ni lini Ukanda huo utarudishwa kwa Wananchi ili waweze kutimiza mahitaji yao madogo madogo.

**22. MHESHIMIWA AUGUSTINO MANYANDA MASELLE (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa sana katika pato la Taifa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitenga Pori la Akiba la Kigosi Mnyovosi kuwa kivutio cha Utalii;

(b) Halmashauri zinazozunguka Mapori ya Akiba zinapaswa kupata asilimia 25 ya mapato ya uwindaji; Je, ni lini Wilaya ya Mbogwe itaanza kulipwa stahili hiyo.

**WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:**

**23. MHESHIMIWA AGRIPINA ZAITUNI BUYOGERA (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula:- Serikali kwa nia njema imewekeza fedha nyingi kwenye miradi mikubwa kama ile ya umwagiliaji Titye na Rungwe Mpya Jimboni Kasulu Vijijini; lakini katika miradi hiyo mpaka sasa Wananchi bado wanalima bila elimu ya kilimo bora na zana duni:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wataalam wa kilimo wa kutosha kuwafundisha Wananchi kilimo cha kisasa ili kufikia malengo na thamani ya miradi hiyo;

(b) Je, ni kwa nini Serikali isiongeze uwezeshaji wa kifedha na vitendea kazi vingine katika Chuo cha Kilimo Mubondo ili miradi hiyo itumike kama maeneo ya mafunzo kwa vitendo kwa kuwafundisha Wakulima moja kwa moja.

**WIZARA YA FEDHA:**

**24. MHESHIMIWA ABASI ZUBERI MTEMVU (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Jiji la Dar es Salaam hasa eneo la Temeke kuna tatizo katika mfumo wa malipo ya EPICA:-

Je, Serikali ina taarifa kuhusu tatizo hilo.

**25. MHESHIMIWA JOHN PAUL LWANJI (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Serikali ilishatoa ahadi ya kuuweka Mkoa wa Singida kenye Awamu ya Pili ya Miradi ya Mpango wa MCC:-

Je, ni miradi gani ya Mkoa huo imeingizwa kwenye mpango wa MCC.

## WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**26. MHESHIMIWA MARIA IBESHI HEWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni vikwazo gani hutokea katika kuandaa Kanuni za Sheria mbalimbali zinazosainiwa na Rais na kusababisha kuchelewesha Kanuni hizo.

**27. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILAGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Akina mama wenye watoto wadogo wanaonyonya wanapohukumiwa jela hufungwa na watoto wao na kifungo hicho huwa cha watu wawili sio mmoja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha hukumu hiyo kwa kuwa inamnyima haki mtoto ambaye hana hatia.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**28. MHESHIMIWA CLARA DIANA MWATUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Karibu vituo vingi vidogo vya Polisi Mtwara havina nyumba za Watumishi ikiwemo na Wakuu wa Vituo na matokeo yake Watumishi hao huishi kwenye nyumba za kupanga kwa wenyeji:-

Je, Serikali haioni kuwa watumishi hao wanaweza kupata kigugumizi pindi wenyeji wao wanapokabiliwa na tuhuma.

**WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**29. MHESHIMIWA JUMA ABDALLAH NJWAYO (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia:- Jimbo la Tandahimba lina maeneo mengi yasiyo na mawasiliano ya uhakika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu kwenye Kata za Michenjele, Mihambwe, Naputa, Namikupa, Mkoreha, Chaume, Nambahu na Ngunja.

**III. HOJA YA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Bajeti pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **28 JANUARI, 2015** | **KATIBU WA BUNGE** |